**SHERIA YA KUTOZA NA KUREKEBISHA BAADHI YA KODI NA KUREKEBISHA SHERIA ZA FEDHA NA SHERIA ZA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA USIMAMIZI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA 2009**

2. Kusomwa.
3. Marekebisho ya kifungu cha 4.
4. Marekebisho ya kifungu cha 23.
5. Marekebisho ya kifungu cha 33.
6. Marekebisho ya kifungu cha 57.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA HOTELI, NAM. 1 YA 1995**

7. Kusomwa.
8. Marekebisho ya kifungu cha 2.
9. Marekebisho ya kifungu cha 3.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA ARDHI, NAM. 12 YA 1992

10. Kusomwa.

11. Marekebisho ya kifungu cha 47.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997

12. Kusomwa.

13. Marekebisho ya kifungu cha 22.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI TAASISI ZA BIASHARA, NAM. 12 YA 2012

14. Kusomwa.

15. Marekebisho ya kifungu cha 24.

**SHERIA NAMBA 4 YA 2019**

**NIMESAINI**

Ahein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

28 Juni..................................................., **2019**

# SHERIA YA KUTOZA NA KUREKEBISHA BAADHI YA KODI NA KUREKEBISHA SHERIA ZA FEDHA NA SHERIA ZA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA USIMAMIZI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma) ya 2019 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya 2009, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**3.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza kifungu kidogo kipya cha (3) na (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

“(3) Iwapo kwa namna yoyote mlipakodi, kwa njia ya zawadi au aina yoyote ya makubaliano, atakubali kutoka kwa mteja au wakala malipo ambayo ni chini ya bei halisi kwa bidhaa zilizouzwa au huduma iliyotolewa, mlipakodi huyo atachukuliwa kuwa amepokea kutoka kwa mteja au wakala malipo ya bei halisi.”

“(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki “bei halisi” maana yake ni kiwango cha fedha ambacho mlipakodi kwa kawaida anahitaji alipwe kutoka kwa mteja au wakala ambaye hana mahusiano naye kwa ajili ya bidhaa au huduma alizozitoa”.

(b) Kuvipa nambari mpya vifungu vidogo vilivyopo vya (3), (4) na (5) kuwa vifungu vidogo vya (5), (6) na (7) kimpangilio.

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**4.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

“(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri, kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi kila baada ya muda, ataamua kiwango cha mauzo ambacho mtu atahitajika kutoa risiti au ankara ya kodi kwa kutumia mashine ya kielektroniki.”

(b) kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

“(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Waziri kwa kushauriana na Kamishna kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi anaweza kumuondoa mtu au kundi la watu katika kutoa risiti au ankara ya kodi kwa kutumia mashine ya kielektroniki.”

(c) kufuta kifungu kidogo cha (5) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (5) kama ifuatavyo:

“(5) Mtu anayetoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya mkono, ataingiza au atapelekea kuingizwa katika stakabadhi hiyo, stakabadhi ya mauzo au ankara ya kodi na kivuli chake, taarifa zifuatazo:

(a) maneno “ankara ya kodi”, “stakabadhi” au “stakabadhi ya malipo” mbele yake;

(b) nambari za mpangilio, nambari ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), nambari ya usajili wa biashara (BRN), jina la biashara, anuani na nambari ya usajili;

(c) jina na anuani ya mteja;

(d) tarehe ya kutolewa ankara ya kodi au stakabadhi;

(e) idadi au ujazo wa bidhaa au huduma zilizotolewa;

(f) bei ya kila bidhaa au huduma na bei ya jumla ya bidhaa au huduma;

(g) kodi iliyotozwa katika muamala; na

(h) muhuri na saini ya mlipakodi au muwakilishi wake.

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**5.** Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kiwango cha riba kitakachotozwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakuwa ni kiwango cha riba ya kukopesha kinachotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwanzoni mwa kila mwaka jumlisha na tano."

Marekebisho ya kifungu cha 57.

**6.** Kifungu cha 57 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Waziri anaweza, kwa kanuni au amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kueleza vigezo, muda na utaratibu wa kupata msamaha ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa kipindi maalum katika mwaka."

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA HOTELI, NAM. 1 YA 1995

Kusomwa.

**7.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi za Hoteli, Nam.1 ya 1995, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**8.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maana ya neno "Meli ya kitalii" katika mpangilio wake kama ifuatavyo:

"Meli ya kitalii" maana yake ni chombo cha baharini ambacho kimetengenezwa kwa ajili ya kutoa huduma za kupokea na kulaza wageni kwa malipo.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**9.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuingiza maneno "meli ya kitalii" baina ya neno "mkahawa" na maneno "uendeshaji wa huduma za kitalii".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA ARDHI, NAM. 12 YA 1992

Kusomwa.

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ardhi, Nam.12 ya 1992, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**11.** Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (5) na kuweka kifungu kidogo kipya cha (5) kama ifuatavyo:

"(5) Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na fedha, anaweza kupanga, kufanya mapitio au, ikiwa ni kwa maslahi ya umma, kupunguza au kusamehe kodi ya ardhi".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997

Kusomwa.

**12.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kamisheni ya Utangazaji Zanzibar, Nam. 7 ya 1997, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**13.** Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta aya (e).

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI WA TAASISI ZA BIASHARA, NAM. 12 YA 2012

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Nam.12 ya 2012, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**15.** Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kila taasisi ya biashara iliyosajiliwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, itachukuliwa kuwa imesajiliwa chini ya Sheria hii, na ndani ya kipindi cha miaka

miwili baada ya Sheria hii kuanza kutumika, itatakiwa kuwasilisha upya taarifa zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii."

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Taasisi ya biashara ambayo imewasilisha upya taarifa zake itapewa nambari mpya ya usajili chini ya masharti ya Sheria hii.

(c) Kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatvyo:

"(3) Endapo taasisi ya biashara yoyote itashindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mrajis atawezesha taasisi ya biashara hiyo kufutwa katika rejista husika."

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 26 Juni, 2019.

.................................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***